







AFRIPRISE
INVESTMENT PLC.

# 2025

www.afriprise.co.tz

# TAARIFA YA KAMPUNI

*Kwenye Mkutano Mkuu wa 20 wa Wanahisa*

AFRIPRISE INVESTMENT PLC.

2025

KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA AFRIPRISE

MKUTANO MKUU WA 20 WA WANAHISA 15-11-2025

# TAARIFA YA KUITISHA
# MKUTANO NA AKIDI

*Wanahisa wanaombwa kuzingatia taarifa iliyotolewa kulingana na kifungu Namba 33 cha Kanuni za Kampuni kinachohusu uitishaji wa Mkutano Mkuu wa Wanahisa.*

*Wanahisa wanaombwa kuzingatia kuwa, akidi kwa mujibu wa kifungu Na. 38 cha Kanuni za Kampuni ni idadi ya wanahisa wasio-pungua 10 wanaomiliki hisa zaidi ya asilimia 50.*

## *TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI*

*Tunapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa Ishirini wa wanahisa wa Kampuni ya Uwekezaji ya Afriprise, utafanyika siku ya jumamosi tarehe 15-11-2025 kwa njia ya mtandao.*

Inapatikana katika tovuti ya Kampuni:
www.afriprise.co.tz

# KUPOKEA AJENDA

*Wanahisa mnaombwa kupokea Ajenda kama zilivyowasilishwa.*



Dondoo Na. 20/2/2025

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI WA WANAHISA WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA AFRIPRISE

Kampuni inapenda kuwajulisha Wanahisa wote kuwa Mkutano Mkuu wa Ishirini wa Wanahisa wa Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE utafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 15/11/2025, kuanzia saa 3:00 Asubuhi, kwa njia ya mtandao. Wanahisa wote watapokea maelekezo ya kujiunga na kushiriki Mkutano kupitia ujumbe wa simu au barua pepe, pamoja na kiungo cha Mkutano.

## DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI (KWA AJILI YA MWAKA WA FEDHA 2024):

1. Kufungua rasmi Mkutano Mkuu wa Ishirini
2. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa
4. Kujadili Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa
5. Kupokea, kujadili na kuridhia:
    a. Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi
    b. Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji
    c. Taarifa ya Wakurugenzi Pamoja na Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2024
6. Kupokea, Kujadili na kuridhia Pendekezo la Gawio kwa mwaka wa fedha 2024
7. Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo la uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2025
8. Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo la Malipo ya Wajumbe wa Bodi kwa mwaka, 2025
9. Kupokea, Kujadili na Kuridhia Pendekezo la Utoaji wa Hisa za upendeleo zisizo na Haki ya Kupiga Kura zenye Uwezo wa Kukombolewa (Non-Voting Redeemable Cumulative Preference Shares)
10. Kupokea na Kujadili mapendekezo rasmi yaliyowasilishwa na Wanahisa
11. Kufunga Mkutano Mkuu

### Maelezo Muhimu kwa Wanahisa:

1. **Mapendekezo toka kwa Wanahisa:** Wanahisa wanahimizwa kuwasilisha mapendekezo yao kwa maandishi kwa Katibu wa Kampuni kabla ya tarehe 10/11/2025 ili yaweze kujumuishwa katika Dondoo namba 10 ya Mkutano.
2. **Taarifa ya Mwaka na Makabrasha:** Taarifa ya Mwaka 2024 pamoja na Makabrasha ya Mkutano yatapatikana kwenye tovuti ya Kampuni kuanzia tarehe 01/11/2025 kupitia anwani: ***https://www.afriprise.co.tz***
3. **Uwakilishi:** Kama Mwanahisa hataweza kuhudhuria Mkutano, anaombwa kuteua mwakilishi kwa kujaza Fomu ya Uwakilishi inayopatikana kwenye tovuti ya Kampuni www.afriprise.co.tz. Fomu zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe: info@afriprise.co.tz au kwa WhatsApp namba: 0757-138048, kabla ya tarehe 14/11/2025, saa 10:00 jioni.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi

**Peter W. Kifunguomali**
Katibu wa Kampuni
Tarehe: **15-11-2025**

# KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TISA WA WANAHISA ULIOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 23/11/2024 KWA NJIA YA MTANDAO.

## 19.1. WALIOHUDHURIA

- Bw. Fortunatus M. Magambo — Mwenyekiti
- Bw. Peter W. Kifunguomali — Katibu

Orodha kamili ya wajumbe pamoja na wawakilishi wa wanahisa waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa uliofanyika siku ya Jumamosi tarehe 23 Novemba 2024 imeambatanishwa kwenye kumbukumbu hizi. Tafadhali angalia Kiambatisho Namba 1.

## 19.2 UFUNGUZI WA MKUTANO

Mwenyekiti, Ndugu. Fortunatus M. Magambo, alifungua Mkutano saa 3:15 Asubuhi kwa kuwakaribisha wanahisa, wafanyakazi pamoja na wageni waalikwa wote waliokuwa wamehudhuria. Alieleza umuhimu wa Mkutano huo katika kutoa tathmini ya mwaka mzima wa utendaji wa Kampuni na kujadili hatua za kimkakati za maendeleo ya baadaye. Aliwataka wanahisa kushiriki kwa ukamilifu katika mijadala.

## 19.3 KUPOKEA NA KURIDHIA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TISA

Wajumbe walipitisha Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa kama zilivyoainishwa kwenye ajenda.

## 19.4 KUPITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA

Katibu, Bw. Peter W. Kifunguomali, aliwasilisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 19 wa Mwaka wa Wanahisa. Kumbukumbu hizo zilisomwa na kupitishwa rasmi bila marekebisho, baada ya wanahisa kuthibitisha kuwa taarifa zilizomo ndizo kumbukumbu sahihi za Mkutano uliopita.

## 19.5 KUPOKEA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE

Maelezo yaliyotolewa kuhusu utekelezaji wa maazimio mbalimbali yaliyopitishwa na kukubaliwa na wanahisa kwenye Mkutano Mkuu wa Kumi na nane uliofanyika 05/08/2024.

## 19.6 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023

### 19.6.1 UWASILISHAJI WA TAARIFA YA MWENYEKITI WA BODI

Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi iliwasilishwa na kujadiliwa. Taarifa hiyo ilihusisha mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023, mwelekeo wa Kampuni katika sekta ya viwanda na miradi mikubwa ya kimkakati. Mwenyekiti alisisitiza dhamira ya Kampuni katika uwajibikaji wa kijamii na uboreshaji wa usimamizi wa rasilimali.

### 19.6.2 UWASILISHAJI WA TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI

Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya kiutendaji iliyojikita katika ukuaji wa mapato, usimamizi wa gharama, maendeleo ya miradi ya kilimo na viwanda na uendelezaji wa mfumo wa kidijitali. Taarifa hiyo ilipokelewa na kupitishwa rasmi na wanahisa.

### 19.6.3 TAARIFA YA WAKAGUZI WA HESABU

Taarifa ya wakaguzi wa nje wa hesabu iliwasilishwa, ikiashiria kuwa hesabu za Kampuni zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. Hakuna dosari kubwa zilizoripotiwa hivyo basi Taarifa hiyo ilipokelewa na kupitishwa.

### 19.6.4 KUPITISHA TAARIFA YA FEDHA YA MWAKA 2023

Wanahisa walipokea na kujadili taarifa ya fedha ya mwaka mzima. Taarifa hii Ilionyesha ongezeko la faida kutokana na utendaji bora na mikakati ya kiuchumi. Taarifa hiyo ilipitishwa kwa kauli moja na wanahisa.

### 19.7 MAAZIMIO KUHUSU GAWIO

Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza gawio la TZS 13 kwa kila hisa kutokana na faida ya mwaka wa fedha 2023. Wanahisa walipokea na kupitisha azimio hilo kwa kauli moja.

### 19.8 KUTEUA WAKAGUZI WA HESABU

Mkutano Mkuu uliridhia kuwa, Kampuni ya ukaguzi ya CROWE Tanzania kuendelea kutoa huduma za ukaguzi kwa mwaka wa fedha wa 2024. Uteuzi huo ulipokelewa na kupitishwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu.

### 19.9 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA PENDEKEZO LA MALIPO YA WAKURUGENZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2025.

Ilielezwa kuwa kuzingatia shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Disemba 31, 2024 Menejimenti inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe kiasi cha Shilingi Milioni Sita na laki mbili (6,200,000/=).
Mkutano Mkuu uliazimia malipo ya Wakurugenzi yawe kiasi cha shilingi Milioni Sita na Laki Mbili (6,200,000/=) kwa kila Mjumbe wa Bodi.

## 19.10 MAPENDEKEZO KUTOKA KWA WANAHISA

Mkutano Mkuu uliarifiwa kuwa, Menejimenti ilipokea barua kutoka PSSSF ikielezea pendekezo la kupunguza idadi ya wajumbe wa bodi kutoka saba (7) na kuwa watano (5) ili kupunguza gharama za uedeshaji wa Kampuni pamoja na gharama za mikutano ya bodi na Kamati zake. Wanahisa ambao wanamikili asilimia arobaini na tano (45%) au zaidi watengewe nafasi mbili (2), wale wanaomiliki kati ya asilimia kumi na tano (15%) hadi ishirini na tisa (29%) watengewe nafasi moja na nafasi mbili watengewe wanahisa wadogowadogo. Pendekezo hili lilipitishwa kwa kauli moja na Mkutano Mkuu.

## 19.11 UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BODI

Uchaguzi ulifanyika kwa ajili ya kuchagua wajumbe wa Bodi kwa kipindi kijacho cha miaka mitatu. Wajumbe wafuatao walichaguliwa na kupitishwa baada ya kupigiwa kura kama ifuatavyo:
Waliopigiwa kura na kupitishwa:

1. Prof. Lucian Ambrose Msambichaka — kura **34,950,053**
2. Ndg. Nathan Edward Mnyawami — kura **34,941,939**
3. Ndg. Magdalena Nelson Mkocha — kura **34,928,325**
4. Ndg. Joseph Matanga Kahungwa — kura **34,925,461**

Kwa mujibu wa maelekezo ya uteuzi, taasisi zifuatazo ziliteua wawakilishi wao kwa ajili ya uwakilishi katika Bodi ya Kampuni kwa kipindi cha miaka mitatu. Uteuzi huu ulithibitishwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu, kama ifuatavyo:

- Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Taasisi hii ilikuwa na nafasi mbili, na iliwateua wajumbe wafuatao:
    - Ndg. Fortunatus M. Magambo
    - Ndg. Valentino M. Daudi

- Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) ilikuwa na nafasi moja, na ilimteua Ndg. Vicent B. Minja

## 19.12 HITIMISHO NA KUFUNGWA KWA MKUTANO

Mkutano ulifungwa rasmi saa 4:19 Asubuhi na Mwenyekiti. Aliwashukuru wanahisa kwa ushiriki wao na akasisitiza dhamira ya Kampuni katika kuongeza thamani kwa wanahisa na kuimarisha taswira ya Kampuni kitaifa na kimataifa

| | |
|---|---|
| ______________________ | ____________________ |
| **Fortunatus M. Magambo** | **Peter W. Kifunguomali** |
| **Mwenyekiti** | **Katibu** |
| Tarehe: 15-11-2025 | Tarehe: 15-11-2025 |

Dondoo Na. 20/3/2025

## KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TISA WA MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 23/11/2024

### WASILISHO

Wanahisa wanaombwa kupokea na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 19 uliofanyika tarehe 23, Novemba, 2024 kama kumbukumbu sahihi:-

### “Azimio la 1/2025


*Imeazimiwa kuwa muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa uliofanyika tarehe 23/11/2024 ni kumbukumbu sahihi.”*

## YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU ULIOPITA

| KUMB | MAELEZO MAFUPI | AZIMIO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| **19.7** | Malipo ya Gawio | Gawio lilipwe Shilingi Kumi na Tatu (13) kwa kila hisa moja. | Gawio lililipwa kwa wanahisa wote waliokamilisha taarifa zao, na malipo yalifanyika tarehe 25 Novemba 2024. |
| **19.8** | Kuteua Mkaguzi wa Mahesabu | Mkutano Mkuu uliidhinisha kampuni ya CROWE Tanzania kuwa wakaguzi wa nje wa hesabu za Kampuni kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2024. | Kampuni ya CROWE Tanzania iliidhinishwa rasmi na ndio iliyokagua Hesabu za Kampuni kwa mwaka 2024 |
| **19.9** | Malipo ya Wakurugenzi | Malipo ya kiasi cha Shilingi 6,200,000/= yalipwe kwa kila mjumbe wa Bodi kwa mwaka fedha ulioishia tarehe 31, Disemba 2024 | Kila Mjumbe wa Bodi alilipwa Kiasi cha Shilingi 6,200,000/= kama ilivyoidhinishwa na Mkutano Mkuu |
| **19.10** | Kupunguza Idadi ya Wajumbe wa Bodi | Idadi ya Wajumbe wa Bodi ipungue kutoka saba (7) wa sasa na kuwa watano (5) | Agizo hili litaanza kutekelezwa baada ya Bodi iliyochaguliwa mwaka 2024 kumaliza muda wake* |
| **19.11** | Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi | Mkutano Mkuu ulichagua wajumbe wanne wa Bodi pamoja na kuidhinisha wajumbe wawili kutoka PSSSF na mjumbe mmoja ambaye ni Rais wa Chemba anaye wakilisha wanahisa wadogo. | Uchaguzi ulifanyika kwa mafanikio. Wajumbe wanne walichaguliwa, pamoja na kuidhinisha wawakilishi wawili wa PSSSF na mjumbe wa TCCIA kama ilivyopendekezwa na kuidhinishwa rasmi na Mkutano Mkuu. |

*Jedwali na. 1*

## KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI NA TAARIFA YA MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2024.



*Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa iko katika Taarifa ya Mwaka.*



## TAARIFA YA MWENYEKITI

*"Furaha haipatikani katika kuwa na pesa tu, bali inatokana na mafanikio katika jitihada na ubunifu." - Franklin Roosevelt*

## TAARIFA YA MWENYEKITI

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Wakurugenzi pamoja na Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE (AFRIPRISE) kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024.

Ninapotafakari safari yetu, nanukuu kauli isemayo: "Mabadiliko si tukio la baadaye, bali ni tukio la sasa." Mwaka 2024 umekuwa ni mwaka wa mageuzi kwa AFRIPRISE - mwaka uliosimamia mikakati, ujasiri katika utekelezaji na kujenga thamani endelevu.

Tulianza mwaka kwa malengo ya kuharakisha mafanikio yaliyotokana na mchakato wetu wa kubadilisha sura ya Kampuni (rebranding) na kuchangamkia fursa mpya za uwekezaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa na Jangwa la Sahara (SADC). Hii imetokana na mafanikio yaliyotokana na zoezi la uuzaji wa hisa za haki mwaka 2023, ambalo Kampuni ilipata TZS bilioni 10, mwaka huu tumeshuhudia mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi, mabadiliko ya muundo wa mali zinazomilikiwa na Kampuni pamoja nafasi ya Kampuni katika masoko ya kikanda.

### MAFANIKIO YA BIASHARA NA UENDELEVU

Katika mazingira ya biashara yenye ushindani na mabadiliko ya haraka, AFRIPRISE imedhihirisha uimara na uwezo wa kujibadilisha. Mkazo wetu katika ukuaji jumuishi na endelevu umeendelea kusukuma mbele mikakati yetu ya uwekezaji salama, bora na rafiki kwa mazingira.

Tumeendelea kuoanisha shughuli zetu na malengo ya ajenda ya maendeleo ya kitaifa, kwa kuhakikisha kuwa kila uwekezaji unaleta faida kwa wanahisa na matokeo chanya kijamii na kiuchumi.

### KUTANGAZA GAWIO

Kwa kutambua utendaji mzuri wa Kampuni na mapato thabiti, Bodi ya Wakurugenzi inapendekeza gawio la TZS 18 kwa kila hisa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024. Pendekezo hili linategemea idhini ya wanahisa katika Mkutano Mkuu huu wa Mwaka. Gawio hili linaonesha uimara wetu kifedha na kuthibitisha dhamira yetu ya kuendelea kuleta thamani kwa wanahisa wetu.

### MTAZAMO WA KIMKAKATI

Tukiangalia mbele, AFRIPRISE imelenga kupanua wigo wake wa uwekezaji katika sekta kubwa

ikiwemo biashara ya kilimo (agribusiness), miundombinu, teknolojia za kifedha (fintech), na teknolojia rafiki kwa mabadiliko ya tabianchi. Tuko tayari kuwa jukwaa bora la uwekezaji kikanda, tukijivunia mtaji imara, utawala bora ulioboreshwa, na ushirikiano ulioimarishwa. Dira yetu ni wazi: Kuwa kichocheo cha mageuzi barani Afrika.

**SHUKRANI**

Mafanikio haya yote yasingewezekana bila usaidizi na ushirikiano wa wadau wetu. Nawashukuru kwa dhati wanahisa wetu kwa imani yao, wadau na washirika wetu kwa kuendelea kutuamini, mamlaka zinazotusimamia kwa mwongozo na ushirikiano wao. Zaidi ya yote, natambua kujituma na uadilifu wa timu ya menejimenti ya AFRIPRISE pamoja na nguvu mpya ya Bodi ya Wakurugenzi. "Tuweke mbegu za maendeleo kwa pamoja, kwa maana mavuno yajayo yatawaletea wengi ustawi wa pamoja."

Ahsanteni sana.

_____________________

Fortunatus Makore Magambo
**Mwenyekiti wa Bodi**
**Tarehe: 15-11-2025**



## TAARIFA YA AFISA MTENDAJI MKUU

*Mpango Mkakati wetu wa mwaka 2023-2025 umefikia hatua muhimu, kwa kuzingatia matakwa ya wadau, kupata faida, uhakika wa mtiririko wa mapato na ongezeko la mapato. Hii inaenda sawia na lengo letu la kuongezeka kitaifa na kimataifa.*

Peter W. Kifunguomali

## TAARIFA YA AFISA MTENDAJI MKUU

Ninayo furaha kuwasilisha taarifa za Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni kuhusu matokeo ya Uwekezaji wa Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024.

### UTANGULIZI

Mpango wetu Mkakati wa mwaka 2023—2025 umefikia mafanikio makubwa, ukiweka mkazo kwenye mafanikio kwa wadau, faida, uhakika wa mtiririko wa fedha na ukuaji wa mapato. Mafanikio haya yameendana na lengo letu la kupanua shughuli zetu kikanda na kimataifa.

### MAFANIKIO YA KIFEDHA

Kampuni imeendelea kukua kwa uthabiti kwa kuongezeka kwa mapato na uwekezaji. Taarifa za fedha kwa mwaka 2024 pamoja na takwimu linganishi za mwaka 2023 ni kama ifuatavyo:

*Jedwali na. 2.* Mgawanyo wa Mfuko wa Uwekezaji hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2024 (kwa maelfu ya TZS):

| MAELEZO | 2024 | 2023 | MABADILIKO (%) |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Uendeshaji | 4,219,666,000 | 3,086,834,000 | +36.7% |
| Matumizi ya Uendeshaji | 1,163,343,000 | 1,049,723,000 | +10.8% |
| Faida Halisi Baada ya Kodi | 3,404,740,000 | 1,976,343,000 | +72.3% |
| Mtaji wa Wanahisa | 52,557,722,000 | 47,524,928,000 | +10.6% |
| Jumla ya mali za Kampuni | 52,692,247,000 | 49,994,556,000 | +5.4% |
| Faida kwa Kila Hisa (EPS) | 23 | 24 | -4.2% |

## MFUKO WA UWEKEZAJI NA KIWANGO CHA FAIDA YA UWEKEZAJI

Mpango wetu wa kupanua uwekezaji umeleta mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kuwekeza kwenye hisa zilizosajiliwa katika Soko la Hisa la Nairobi. Thamani ya mali halisi za Kampuni ni TZS bilioni 52, ikiwa ni ongezeko la 10% ikilinganishwa na TZS bilioni 47 kufikia tarehe 31 Desemba 2023. Hivyo, kiwango cha wastani cha ukuaji wa mali halisi kwa mwaka ni 10%.

Mfuko wa uwekezaji umeongezeka kwa 23% kutoka TZS bilioni 42 kufikia tarehe 31 Desemba 2023 hadi TZS bilioni 49 kufikia 31 Desemba 2024. Sehemu kubwa ya uwekezaji ni kwenye hati fungani za serikali kwa 36%, hisa kwa 61% na mali nyingine kwa 3%. Mafanikio haya yametokana kwa kiasi kikubwa na ufanisi wa uendeshaji wa Kampuni pamoja na mpango mkakati wake wa kupanua uwekezaji.

Faida kwa kila hisa ni TZS 23.33 ikilinganishwa na TZS 24 mwaka 2023. Kuongezeka kwa faida mwaka jana kulitokana na kuongeza idadi ya hisa kupitia toleo la hisa za haki (rights issue) ambalo liliongeza idadi ya hisa kwa 100%.

Aidha, faida ya uwekezaji (Return on Investment) ni 7% ikilinganishwa na 5% mwaka 2023, kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji mwaka huu na matarajio ya kupata faida zaidi katika miaka ijayo.

*Jedwali na. 3*

| AINA YA UWEKEZAJI | 2024 | % | 2023 | % |
|---|---|---|---|---|
| Hati fungani za Serikali | 15,680,721 | 32 | 15,037,876 | 36 |
| Uwekezaji katika Hisa | 30,949,793 | 63 | 25,357,243 | 61 |
| Amana za muda mfupi | 305,000 | 1 | 305,000 | 1 |
| Mali zisizohamishika | 1,155,000 | - | 221,347 | - |
| Hati fungani za Makampuni (Corporate Bonds) | 1,200,000 | 3 | 750,000 | 2 |
| **Jumla** | **49,290,514** | **100** | **41,671,466** | **100** |

## MATARAJIO KWA MWAKA UJAO

Tunatarajia kupanua uwekezaji wetu katika hisa nje ya Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na Nairobi (NSE), tukilenga hisa zinazotoa faida na ukuaji wa thamani ili kuongeza mapato. Pia, tunafanya mabadiliko katika kupanua uwekezaji kwenye hisa, hati fungani, na masoko ya fedha ili kupunguza athari na kuongeza mapato kwenye Kampuni.

Vilevile, tunaendelea kufanya utafiti na kuchunguza fursa mpya za biashara zinazojitokeza.

## HITIMISHO

Nawashukuru Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi,
timu ya menejimenti, mabenki yetu, wakaguzi, na wawekezaji kwa ushirikiano wao. Kwa juhudi zetu za pamoja, Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE itaendelea kustawi.

Ahsanteni sana.

**Peter William Kifunguomali,**
Afisa Mtendaji Mkuu
**Tarehe: 15-11-2025**

## TAARIFA YA UENDELEVU

Taarifa hii ya uendelevu inaelezea juhudi na mafanikio ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE katika kukuza uendelevu na utekelezaji wa uwekezaji unaozingatia uwajibikaji. Dhamira yetu kwa misingi ya mazingira, kijamii, na utawala bora (ESG) ndiyo inayotuongoza katika shughuli zetu na maamuzi ya uwekezaji. Taarifa hii inahusisha hatua kuu za uendelevu zilizotekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2024.

### UWAJIBIKAJI WA KIMAZINGIRA

1. Ufanisi wa Matumizi ya Nishati
    - Tumeanzisha hatua za kuokoa nishati katika ofisi zetu, hali iliyopelekea kupungua kwa matumizi ya nishati kwa asilimia 15 ikilinganishwa na mwaka uliopita.
    - Mfuko wetu wa uwekezaji unajumuisha makampuni yenye sera madhubuti za kimazingira.

2. Kupunguza Taka
    - Jitihada za kidijitali zimepunguza matumizi ya karatasi kwa asilimia 25, ikiwa ni sehemu ya malengo yetu ya kupunguza athari za kimazingira.

Majukumu ya kijamii

1. Ushirikishwaji wa Jamii
    - Tunayo programu ya misaada ambapo sehemu ya faida yetu hutolewa kwa taasisi za misaada na miradi ya jamii, hasa kwenye sekta ya elimu na afya. Mwaka 2024, tulitoa msaada kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kulelea wazee Bagamoyo.
    - Wafanyakazi wetu walishiriki katika kazi za kujitolea kusaidia miradi mbalimbali ya kijamii

### USTAWI WA WAFANYAKAZI

- Tunatoa programu kamili za afya na ustawi kwa wafanyakazi wetu, ikiwa ni pamoja na huduma za afya ya akili na uchunguzi wa afya wa mara kwa mara.
- Dhamira yetu ya usawa na ujumuishaji inaakisiwa na uwiano wa kijinsia kazini, ambapo asilimia 50 ya wafanyakazi ni wanawake. Pia, wanawake wanawakilishwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi.

### UTAWALA BORA (GOOD GOVERNANCE)

1. Maadili ya Uwekezaji
    - Maamuzi yetu ya uwekezaji yanazingatia mfumo madhubuti wa ESG, kuhakikisha tunaunga mkono biashara zenye maadili bora.
    - Tunafanya tathmini za ESG mara kwa mara kwa makampuni tuliyowekeza kuhakikisha ufuatiliaji na maboresho ya kudumu.

2. Uwajibikaji na Uwazi

- Tumeweka mfumo wa uwazi wa utoaji wa taarifa, unaowapa wadau wetu taarifa za mara kwa mara kuhusu jitihada zetu za uendelevu.

## MALENGO YA UENDELEVU KWA MWAKA UJAO

1. Mazingira
    - Kupunguza zaidi matumizi ya nishati kupitia mifumo ya kisasa ya usimamizi wa nishati iliyoidhinishwa.
    - Kuongeza kiwango cha uwekezaji katika miradi ya nishati mbadala.

2. Jamii
    - Kupanua programu ya ushirikiano wa kijamii kwa kushirikiana na taasisi za elimu ili kutoa ufadhili wa masomo.
    - Kuboresha programu za mafunzo kwa wafanyakazi ili kutoa fursa zaidi za kukuza taaluma.

3. Utawala bora

    - Kuimarisha vigezo vya tathmini ya ESG kwa kuongeza vipimo madhubuti vya athari za kijamii.
    - Kuboresha mfumo wa kushirikisha wadau kwa kuzingatia maoni na mapendekezo yao katika mkakati wa uendelevu.

## TAARIFA YA BODI YA WAKURUGENZI

Wajumbe wa bodi (wakurugenzi) wanayo furaha kuwasilisha taarifa yao kuhusu taarifa za Hesabu za Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024. Taarifa hii inaelezea hali halisi ya Kampuni kwa kipindi chote cha mwaka 2024.

### 01. USAJILI

Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE (AFRIPRISE) imesajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 kama kampuni ya umma yenye dhima ya kikomo. Kampuni hii imesajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na ina makazi yake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 02. AINA YA BIASHARA

Shughuli kuu za Kampuni ni usimamizi wa uwekezaji, haswa kwenye hisa za makampuni yaliyoorodheshwa, ikiwa ni pamoja na hati fungani za makampuni yenye historia ya kutoa faida, pamoja na hati fungani za serikali na uwekezaji kwenye maghala yaliyo maeneo ya kimkakati. Aidha, Kampuni inahamasisha utamaduni wa kuweka akiba miongoni mwa wanahisa wake kupitia uwekezaji katika makampuni yanayofanya vizuri.

### 03. MAADILI YA MSINGI

- Uwajibikaji
- Uaminifu
- Ushirikiano
- Ubunifu

## MAONO, DHIMA, KAULI MBIU NA MAADILI KATIKA KAZI

**DHAMIRA**

Kuwaongezea wanahisa thamani ya muda mrefu kwa kutoa faida bora iliyozingatia usalama na uendelevu wa uwekezaji.

**DIRA**

Kuwa mtoa huduma bora wa usimamizi wa uwekezaji nchini Tanzania.

**KAULI MBIU**

"Pamoja tuna nguvu zaidi."

### 04. TATHMINI YA MATOKEO YA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI

Taarifa ya Mahesabu imeandaliwa kwa kufuata viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (IFRS) pamoja na matakwa ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Sera za uhasibu zimetumika kwa mfuatano kama mwaka uliopita.

*Jedwali na. 4:* **Hakukuwa na mabadiliko ya mtaji wa hisa zilizoidhinishwa wala zilizotolewa katika mwaka wa taarifa.**

| | | | IDADI YA HISA | |
|---|---|---|---|---|
| Idadi ya hisa zilizoidhinishwa: | | | **2024** | **2023** |
| Hisa za Kawaida (Ordinary Shares) | | | 5,000,000,000 | 5,000,000,000 |
| | | | | |
| | **2024** | **2023** | **2024** | **2023** |
| | Shs'000 | Shs'000 | **Idadi ya Hisa** | |
| Hisa za Kawaida (Ordinary Shares) | 2,918,306 | 145,915,320 | 145,915,320 | 72,957,660 |
| Mapato ya Hisa (Share Premium) | 9,828,506 | 708,799 | - | |
| | **12,746,812** | **2,167,952** | **145,915,320** | **72,957,660** |

Kampuni ilipata faida halisi baada ya kodi ya TZS 3,404,740,000 kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2024, ikilinganishwa na TZS 1,976,343,000 mwaka uliopita. Mapato ya Kampuni yaliongezeka kwa asilimia 11 kutoka TZS 3,086,834,000 mwaka uliopita hadi TZS 4,219,666,000. Ongezeko hili lilitokana na ongezeko la mapato ya gawio kufuatia maamuzi ya bodi ya kupanua wigo wa uwekezaji.

## 05. GAWIO

Bodi inapendekeza gawio la Shilingi 18 kwa kila hisa, sawa na jumla ya Shilingi 2,626,475,760 ukilinganisha na gawio la Shilingi 13 kwa kila hisa sawa na jumla shilingi 1,896,899,160 kwa mwaka uliopita 2023.

## 06. MALENGO YA KIMKAKATI

- **Kuongeza thamani kwa wanahisa:** Kuhakikisha Kampuni inatimiza malengo yake mara kwa mara.
- **Ubora wa uwekezaji;** Kuongeza mapato ya uwekezaji kwa 22% kila mwaka.
- **Ubora wa uendeshaji;** Kuboreshautendaji kwa wafanyakazi wake waliopo kupitia teknolojia sahihi ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji; kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja, kuongeza utiifu wa taasisi; kuboresha utamaduni wa Kampuni; kuboresha ustawi wa wafanyakazi, na kuongeza ufanisi na tija kwa wafanyakazi. Kampuni inatarajia kufikia uwiano wa ubora wa kiutendaji wa asilimia 95.

## 07. BODI YA WAKURUGENZI

Majina ya Wakurugenzi waliopo hadi tarehe ya taarifa hii::

| JINA LA MKURUGENZI | NAFASI | ELIMU | URAIA | MABADILIKO |
|---|---|---|---|---|
| Ndg. Fortunatus Makore Magambo | Mwenyekiti | Mchumi | Mtanzania | |
| Prof. Lucian A. Msambichaka | Mjumbe | Mchumi | Mtanzania | |
| Ndg. Joseph Matanga Kahungwa | Mjumbe | Mhasibu | Mtanzania | |
| Bi. Magdalenaa N. E. Mkocha | Mjumbe | Kilimo/Mchumi | Mtanzania | |
| Ndg. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | Mchumi | Mtanzania | |
| Ndg. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | Ununuzi na Ugavi | Mtanzania | *Alijiuzulu 23 Nov 2024* |
| Ndg. Paul F. Koyi | Mjumbe | TEKNOHAMA | Mtanzania | *Alijiuzulu 23 Nov 2024* |
| Vicent B. Minja | Mjumbe | Mhasibu | Mtanzania | *Aliyechaguliwa* |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | *23 Nov 2024* |
| Valentino M. Daudi | Mjumbe | Wakili | Mtanzania | *Aliyechaguliwa 23 Nov 2024* |

Pia kuna wakurugenzi wanaowakilisha taasisi zilizowekeza kwenye kampuni, mfano:

- Fortunatus M. Magambo na Ernest Khisombi wanawakilisha Public Service Social Security Fund (PSSSF) yenye hisa 65,661,894.

## 08. UTAWALA BORA

Bodi ina jukumu la juu la kuongoza kampuni na kuhakikisha uwekezaji mkubwa, hatari na sera za ndani zinafuatiliwa kwa ufanisi. Mwaka 2024, bodi ilikutana mara 6 (Mikutano minne (4) ya kawaida na miwili (2) ya dharura).

*Jedwali na. 5:* **Mahudhurio ya Wakurugenzi kwa mwaka 2024:**

| NA. | JINA | NAFASI | IDADI YA VIKAO | IDADI YA VIKAO ALIVYOHUDHURIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Fortunatus M. Magambo | Mwenyekiti | 6 | 6 |
| 2. | Prof. Lucian A. Msambichaka | Makamu Mwenyekiti | 6 | 6 |
| 3. | Bw. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | 6 | 6 |
| 4. | Bi. Magdalena N. E. Mkocha | Mjumbe | 6 | 6 |
| 5. | Bw. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | 6 | 6 |
| 6. | Bw. Paul F. Koyi | Mjumbe | 6 | 2 |
| 7. | Bw. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | 6 | 6 |

## 09. KAMATI ZA BODI:

- Kamati ya Uwekezaji: Prof. Msambichaka (Mwenyekiti), Nathan Mnyawami, Paul Koyi
- Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Athari: Joseph Kahungwa (Mwenyekiti), Ernest Khisombi, Magdalenaa Mkocha. Kila kamati ilifanya mikutano 4 mwaka 2024.

## 10. KAZI KUU ZILIZOFANYWA NA BODI:

- Mapitio ya taarifa za ukaguzi na uwekezaji
- Kupunguza gharama na kuongeza mapato
- Kuandaa na kupitisha bajeti na mpango mkakati wa mwaka 2025
- Kupitia miradi mipya
- Tathmini ya hatari (kifedha, kimkakati, ESG)

*Jedwali na. 6*

| MUUNDO WA UMILIKI WA HISA | ASILIMIA | SHS'000 |
|---|---|---|
| | | |
| PSSSF | 45 | 1,313,238 |
| Abbasi Export Ltd | 13 | 387,746 |
| Joyce Mwita Gachuma | 5 | 150,000 |
| Christopher Mwita Gachuma | 4 | 116,732 |
| Amin Mohamed Valji | 2 | 42,200 |
| Wanahisa wengine (chini ya 1.5) | 31 | 908,390 |
| | **100** | **2,918,306** |

## 11. UZINGATIAJI WA SHERIA NA KANUNI

Kampuni ilidumisha uhusiano mzuri na taasisi muhimu za udhibiti kama TRA, CMSA, DSE n.k. na ilifuata kikamilifu sheria zote husika.

## 12. UHAKIKA WA TAARIFA ZA KIFEDHA

Kampuni ina wafanyakazi mahiri kwenye idara ya fedha na uhasibu, na taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango wa kimataifa vya uandaaji wa taarifa Mahesabu

## 13. MUUNDO WA MTAJI WA KAMPUNI

Mtaji ulioruhusiwa: TZS 100,000,000,000 (hisa 5,000,000,000 za TZS 20 kila moja)
Mtaji uliolipwa: TZS 12,746,812,000

## MUUNDO WA UMILIKI WA HISA:

## 14. TAARIFA KUHUSU SOKO LA HISA

Kampuni imesajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Bei ya hisa kufikia tarehe 31 Desemba 2024 ilikuwa TZS 215 ukilinganisha na shilingi 190 kwa mwaka 2023 huku thamani ya soko (market capitalization) ikiwa TZS 31,371,793,800 ikilinganishwa na Shilingi 27,723,911,000 kwa mwaka 2023.

## 15. BIASHARA ENDELEVU

Majadiliano ya Bodi kuhusu ukuaji endelevu hayazingatii vipimo vya kifedha pekee. Bodi huzingatia masuala mapana ya uendelevu, ikiwemo mabadiliko ya tabianchi na matumizi salama ya malighafi ya
Kampuni:

- Kujiepusha kufadhili miradi au biashara zinazoathiri mazingira, hata kama zina faida kifedha;
- Kuhamasisha matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira;
- Kuhimiza biashara za mtandaoni (e-commerce);
- Kuanzisha mfumo wa ndani wa usimamizi wa mazingira kwa kutumia teknolojia;
- Kutoa elimu na uhamasishaji kupitia

majukumu ya kijamii ya Kampuni (CSR)

## 16. KUENDELEA KWA SHUGHULI (GOING CONCERN)

Wakurugenzi wanaamini kuwa Kampuni ina uwezo wa kifedha kwa kuiwezesha kuendelea na shughuli zake za biashara kwa kipindi kijacho. Taarifa za fedha zimeandaliwa kwa misingi ya "uendelevu". Hakuna mabadiliko makubwa yanayotarajiwa ambayo yanaweza kuathiri shughuli za Kampuni kwa sasa.

## 17. USTAWI WA WAFANYAKAZI

### MAFUNZO

Kampuni hutoa udhamini kwa mafunzo ya muda mfupi nchini na nje ya nchi kulingana na mahitaji ya Kampuni na uwezo wa kifedha. Pia huunga mkono juhudi binafsi za wafanyakazi kwa

mafunzo ya muda mrefu.

### MIKOPO MIKUBWA NA MIDOGO

Kampuni hutoa mikopo ya mshahara kwa wafanyakazi kusaidia mahitaji yao ya kifedha, kwa kufuata masharti yaliyowekwa na bajeti ya mwaka husika.

### MSAADA WA KIFEDHA

Kampuni hutoa msaada wa kifedha pale ambapo mfanyakazi au mtegemezi wake wa karibu akifariki dunia.

### MAFAO YA KUSTAAFU

Kampuni huchangia katika mifuko ya pensheni inayosimamiwa na serikali kama vile PSSSF kwa niaba ya wafanyakazi wake wote.

### WATU WENYE ULEMAVU

Kampuni hutoa fursa sawa kwa watu wenye ulemavu kwa nafasi ambazo wana uwezo wa kuzitimiza.

### HUDUMA ZA MATIBABU

Kampuni ina mkataba na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kutoa huduma ya bima ya afya kwa wafanyakazi na wategemezi wao wa karibu.

## 18. USAWA WA JINSIA

Hadi tarehe 31 Desemba 2024, Kampuni ilikuwa na wafanyakazi 6 ambayo ni sawa na mwaka 2023 yaani wanaume 3 na wanawake 3.

## 19. MASUALA YA MAZINGIRA, JAMII NA UTAWALA (ESG)

Kampuni inatilia mkazo zaidi vipengele vya masuala ya mazingira, jamii na utawala bora na imeanzisha njia bora zaidi za kupima mafanikio yake. Kampuni imejiwekea lengo la kufanya kazi kwa kutumia mifumo isiyotegemea karatasi (paperless environment), na kuwekeza kwenye kampuni zinazozingatia usalama wa mazingira.

## 20. MAENDELEO YA BAADAYE

Tangu mwaka 2018, bodi ya wakurugenzi iliamua kuanza kupanua wigo wa uwekezaji kwa kuwekeza katika bidhaa nyingine mbali na hisa. Licha ya kuwa zaidi ya 95% ya uwekezaji wa Kampuni tangu 2005 ulikuwa kwenye hisa za makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, bodi imeelekeza nguvu kwenye hati fungani, dhamana za serikali, na amana za benki zenye riba kwa sababu ya utulivu wa mapato.

Bodi pia inatafiti fursa zingine kama biashara ya uagizaji na usafirishaji wa bidhaa, biashara ya mifugo, na bidhaa za kifedha kama biashara ya hati fungani.

## 21. ULINZI WA MALI ZA KAMPUNI

Bodi ya wakurugenzi inawajibika kulinda mali za Kampuni. Imeidhinisha sera mbalimbali kama vile sera za kifedha na uwekezaji ili kuimarisha udhibiti wa ndani. Sera hizi hufanyiwa marekebisho mara kwa mara ili kuendana na mazingira ya biashara. Hakuna tukio kubwa la udanganyifu lililoripotiwa mwaka 2024.

## 22. MIAMALA NA MAHUSIANO NA WADAU WA KARIBU

Miamala yote na wadau wa karibu (related parties) imeelezwa kwenye Kumbukumbu Na. 35 ya taarifa za fedha.

## 23. WAJIBU WA WALE WENYE MAMLAKA YA UTAWALA

Wakurugenzi wana jukumu la kuhakikisha kuwa taarifa za kifedha zinaonyesha hali halisi ya kampuni, matokeo ya shughuli zake, na mtiririko wa fedha kwa kipindi husika kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya taarifa za kifedha (IFRS) na sheria husika za Tanzania. Pia wanathibitisha kuwa kampuni inazingatia TFRS 1 na sheria zote nyingine husika.

Taarifa hizi za kifedha zilizoko kuanzia ukurasa wa 22 hadi 64 ziliidhinishwa na bodi ya wakurugenzi siku ya:

Tarehe: Jumatatu, 30 Juni 2025

Waliotia saini kwa niaba ya Bodi:

Fortunatus Makore Magambo
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** 25 Juni 2025

Prof. Lucian Ambrose Msambichaka
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** 25 Juni 2025

# TAARIFA YA
# WAJIBU WA WAKURUGENZI

Wakurugenzi, kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, wanatakiwa kudumisha kumbukumbu sahihi za uhasibu na wanawajibika kwa usahihi na uadilifu wa taarifa za kifedha na taarifa nyingine zinazohusiana zilizomo katika taarifa hii.

Ni wajibu wao kuhakikisha kuwa taarifa za kifedha zinaonyesha kwa usahihi hali halisi ya Kampuni kufikia mwisho wa mwaka wa fedha na matokeo ya shughuli zake pamoja na mtiririko wa fedha kwa kipindi hicho, kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha (IFRS). Wahasibu wa nje wameajiriwa kutoa maoni huru juu ya taarifa hizo za kifedha.

Taarifa ya fedha imeandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu na zinatokana na sera za uhasibu zinazofaa, zilizotumika kwa uthabiti na kuungwa mkono na maamuzi na makadirio ya tahadhari.

Wakurugenzi wanatambua kuwa wao ndio wenye wajibu wa mwisho wa kuhakikisha kuwepo kwa mfumo wa udhibiti wa kifedha wa ndani ya Kampuni na wanatilia mkazo umuhimu wa kudumisha mazingira imara ya udhibiti. Ili kuwasaidia kutimiza wajibu huu, bodi ya wakurugenzi huweka viwango vya udhibiti wa ndani vinavyolenga kupunguza hatari ya makosa au hasara zinazoweza kujitokeza.

Viwango hivi vinajumuisha ugawaji wa majukumu ndani ya mfumo unaoeleweka vyema, taratibu madhubuti za uhasibu, na mgawanyo wa kazi unaokidhi viwango vya kukubalika vya udhibiti wa athari.

Udhibiti huu hufuatiliwa katika Kampuni nzima na wafanyakazi wote wanatakiwa kudumisha viwango vya juu vya maadili ili kuhakikisha kuwa biashara ya Kampuni inaendeshwa kwa njia inayokubalika kijamii na kimaadili. Mkazo wa usimamizi wa hatari ndani ya kampuni uko kwenye kutambua, kupima, kudhibiti na kufuatilia aina zote zinazojulikana za athari.

Ingawa athari za uendeshaji haziwezi kuondolewa kabisa, Kampuni hujitahidi kuzipunguza kwa kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu sahihi, udhibiti, mifumo, na mienendo ya kimaadili kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

Wakurugenzi wanaamini, kutokana na taarifa na maelezo waliyopewa na menejimenti, kuwa mfumo wa udhibiti wa ndani unatoa uhakika wa kutosha kuwa rekodi za kifedha zinaweza kutegemewa katika maandalizi ya taarifa za kifedha. Hata hivyo, mfumo wowote wa udhibiti wa kifedha wa ndani unaweza kutoa uhakika wa kutosha tu, na si kamili, dhidi ya makosa au hasara kubwa.

Wakurugenzi wamekagua makadirio ya mtiririko wa fedha wa Kampuni kwa mwaka hadi 31 Desemba 2025 na kwa kuzingatia mapitio hayo pamoja na hali ya sasa ya kifedha, wamethibitisha kuwa Kampuni ina rasilimali za kutosha kuendelea na shughuli zake kwa kipindi kijacho.

Wahasibu wa nje wanawajibika kwa kufanya ukaguzi wa uhuru na kutoa maoni yao kuhusu taarifa za kifedha za Kampuni. Taarifa za kifedha zimekaguliwa na wahasibu wa nje na taarifa yao imewasilishwa katika kurasa 26 hadi 30.

Taarifa za kifedha zilizomo katika kurasa 22 hadi 64, ambazo zimeandaliwa kwa misingi ya kuendelea na shughuli (going concern), ziliidhinishwa na bodi ya wakurugenzi tarehe ya taarifa hii na kusainiwa kwa niaba yao na:

-------------------------
Fortunatus Makore Magambo
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** 25 Juni 2025

------------------------------
Prof. Lucian Ambrose Msambichaka
**Mkurugenzi**
**Tarehe:** 25 Juni 2025

# TAMKO LA MKUU IDARA YA UHASIBU
# TAMKO LA MKUU IDARA YA FEDHA/UHASIBU WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA AFRIPRISE

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), kwa mujibu wa mamlaka iliyotolewa chini ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi Na. 33 ya 1972, iliyorekebishwa kwa Sheria Na. 2 ya 1995, inahitaji taarifa za kifedha ziambatane na tamko lililotolewa na Mkuu wa Idara ya Fedha/Uhasibu wa taasisi husika.

Ni jukumu la Mhasibu Mtaalamu kusaidia Bodi ya Wakurugenzi/Baraza la Usimamizi/Menejimenti kutekeleza wajibu wao wa kuandaa taarifa za kifedha zinazoonyesha ukweli na usahihi wa hali ya kifedha na utendaji wa taasisi kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu na matakwa ya kisheria.

Wajibu wa mwisho wa kisheria wa kuandaa taarifa za kifedha unabaki kuwa wa Bodi ya Wakurugenzi/Baraza la Usimamizi kama ilivyobainishwa kwenye sehemu ya "Wajibu wa Wakurugenzi" hapo awali.

Mimi, Joel Chikoma, nikiwa Mkuu wa Idara ya Fedha/Uhasibu wa Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kufikia tarehe 31 Desemba 2024 na kwa mwaka huo, ninatambua wajibu wangu wa kuhakikisha kuwa taarifa za kifedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango husika vya uhasibu na masharti ya sheria.

Kwa hiyo, ninathibitisha kuwa taarifa za kifedha zinaonyesha hali halisi na ya kweli ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kufikia tarehe hiyo, na kwamba zimeandaliwa kwa kuzingatia rekodi za kifedha zilizohifadhiwa ipasavyo.

Jina: **Joel Chikoma**
Sahihi: 

Nafasi: **Head of Finance**
NBAA Membership No: **ACPA 3285**
**Tarehe:** 25 Juni 2025



# TAARIFA YA MAHESABU

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI

## YA MWAKA WA FEDHA ULIOISHA 31/12/2024

| | 2024<br>Shilingi' 000 | 2023<br>Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| Mapato | 4,219,666 | 3,086,834 |
| Mapato anuwai | 466,937 | 159,304 |
| Mapato mengine/ (hasara) ya uendeshaji | - | 184,951 |
| Matumizi ya uendeshaji | (1,163,343) | (1,049,723) |
| **Faida ya uendeshaji** | **3,523,260** | **2,381,366** |
| Gharama za kifedha | (10,079) | (345,233) |
| **Faida/ (hasara) kabla ya kodi** | **3,513,181** | **2,036,133** |
| Kodi | (108,441) | (59,790) |
| Faida/(Hasara) kwa mwaka | **3,404,740** | **1,976,343** |
| **Mapato mengine kamili:**<br>**Vitu ambavyo havitawekwa upya kwenye faida au hasara** | | |
| Kupanda/ (kushuka) kwa thamani ya hisa | 3,533,903 | 4,181,980 |
| **Mapato/(hasara) mengine ya mwaka** | 3,533,903 | 4,181,980 |
| **Jumla ya mapato/(hasara) kwa mwaka** | **6,938,643** | **6,158,323** |
| **Faida kwa kila hisa** | **23.33** | **25.23** |

# TAARIFA YA WARAKA KAMA

# ILIVYOKUWA HADI TAREHE 31/12/2024

| | 2024 Shilingi' 000 | 2023 Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| **Rasilimali** | | |
| **Rasilimali za muda mrefu** | | |
| Mali ya kudumu inayogusika | 115,766 | 109,068 |
| Uwekezaji wa kwenye ardhi/majengo | 221,347 | 221,347 |
| Haki ya matumizi ya rasilimali | 40,553 | 59,711 |
| Rasilimali zisizogusika | 1,027 | 3,040 |
| Mikopo | 47,957 | 73,173 |
| Uwekezaji wa kwenye hisa | 30,949,793 | 25,357,243 |
| Dhamana za serikali | 15,680,721 | 15,037,876 |
| Uwekezaji mwingine wa kifedha | 1,200,000 | 600,000 |
| | **48,257,164** | **41,461,458** |
| **Rasilimali za muda mfupi** | | |
| Mikopo | 36,340 | 28,954 |
| Rasilimali za biashara | 669,164 | 1,036,105 |
| Kodi ya muda mfupi | 333,423 | 308,164 |
| Uwekezaji mwingine wa kifedha | 1,155,000 | 455,000 |
| Fedha na thamani ya fedha | 2,241,156 | 6,704,875 |
| | **8,533,098** | **1,450,106** |
| **Jumla ya Rasimali** | **52,692,247** | **49,994,556** |
| **Mtaji na Madeni** | | |
| Mtaji | 12,746,812 | 12,746,812 |
| Jumla ya akiba | 14,912,266 | 12,559,826 |
| Faida kuu | 24,898,644 | 22,218,290 |
| | **52,557,722** | **47,524,928** |
| **Madeni ya muda mrefu** | | |
| Mkopo wa muda mrefu | - | 1,885,443 |
| Dhima ya kukodisha | - | 32,944 |
| Kodi iliyoahirishwa | 1,784 | 1,784 |
| | **1,784** | **1,920,171** |
| **Madeni ya muda mfupi** | | |
| Madeni ya biashara | 36,541 | 200,758 |
| Mkopo wa muda mfupi | - | 272,398 |
| Gawio | 47,406 | 51,922 |
| Dhima ya kukodisha | 48,794 | 24,379 |
| | **132,741** | **549,457** |
| **Jumla ya madeni** | **134,525** | **2,469,628** |
| **Jumla ya mtaji na madeni** | **52,692,247** | **49,994,556** |

# TAARIFA YA MABADILIKO
# YA MTAJI KWA MWAKA 2024

| | Mtaji wa hisa Shilingi' 000 | Mapato ya hisa Shilingi'000 | Akiba ya thamani ya uwekezaji kwenye hisa Shilingi'000 | Gharama uuzaji wa hisa Shilingi'000 | Jumla ya hifadhi nyingine na gharama za uuzaji wa hisa | Faida kuu Shilingi'000 | Jumla ya mtaji 000' |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka uliopita | | | | | | | |
| Mtaji wa hisa kuanzia tarehe 1/1/2023 | 1,459,153 | 708,799 | 9,512,950 | (629,662) | 8,883,288 | 21,277,813 | 32,329,05 |
| Faida ya mwaka | | | | | | 1,976,343 | 1,976,343 |
| Mapato mengine | | | 4,181,980 | | 4,181,980 | | 4,181,980 |
| Mauzo ya hisa za upendeleo | 1,459,153 | 9,119,707 | | | | | 10,578,860 |
| Gharama za mauzo ya hisa | | | | | | | (599,426) |
| Kuhamisha kwenda akiba kuu | | | | (599,426) | (599,426) | | (599,426) |
| Gawio | | | 93,984 | | 93,984 | (87,414) | 6,568 |
| Kodi ya zuio miaka ya nyuma | | | | | | (948,450) | (948,450) |
| **Mtaji wa hisa kuanzia 31/12/2023** | **2,918,306** | **9,828,506** | **13,788,914** | **(1,229,088)** | **12,559,826** | **22,218,288** | **47,524,926** |
| **MWAKA HUU** | | | | | | | |
| **Mtaji wa hisa kuanzia tarehe 1/1/2023** | **2,918,306** | **9,828,506** | **13,788,914** | **(1,229,088)** | **12,559,826** | **22,218,288** | **47,524,926** |
| Faida ya mwaka | | | | | | 3,404,740 | 3,404,740 |
| Mapato mengine | | | 3,533,903 | | 3,533,903 | | 3,533,903 |
| Mauzo ya hisa za upendeleo | | | | | | | |
| Gharama za mauzo ya hisa | | | | | | | |
| Kuhamisha kwenda akiba nyingine | | | (1,181,463) | | (1,181,463) | 1,181,463 | |
| Gawio | | | | | | (1,905,847) | (1,905,847) |
| **Mtaji wa hisa kuanzia tarehe 31/12/2024** | **2,918,306** | **9,828,506** | **16,141,354** | **(1,229,088)** | **24,898,644** | **24,898,644** | **52,557,722** |

# TAARIFA YA

# MTIRIRIKO WA FEDHA

| | 2024<br>Shilingi' 000 | 2023<br>Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uendeshaji** | | |
| Fedha toka kwenye shughuli za uendeshaji | 3,795,465 | 1,296,072 |
| Gharama za kifedha | (10,079) | (345,233) |
| Kodi iliyolipwa | (133,700) | (80,958) |
| **Fedha taslimu inayotokana na uendeshaji** | **3,651,686** | **869,881** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na uwekezaji** | | |
| Manunuzi ya mali ya kudumu inayogusika | (37,467) | (16,928) |
| Manunuzi ya Haki ya kutumia Rasilimali | (74,866) | (57,323) |
| Manunuzi ya Rasilimali Isiyogusika | - | (2,053) |
| Uondoaji wa mali ya haki ya matumizi | 57,322 | - |
| Manunuzi ya amana za serikali | (2,058,647) | (1,549,229) |
| Mtiririko kwenye uwekezaji katika hisa | (3,214,829) | (3,214,829) |
| Mikopo | 17,830 | (40,399) |
| Manunuzi ya uwekezaji mwingine wa kifedha | (1,300,000) | (570,000) |
| Mauzo ya uwekezaji katika hisa | 2,571,985 | 1,951,047 |
| **Fedha taslimu iliyotumika katika uwekezaji** | **-4,038,672** | **(3,499,714)** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na mtaji** | | |
| Mauzo ya hisa za upendeleo | - | 10,578,860 |
| Mtiririko wa mkopo | (2,157,841) | (239,101) |
| Mtiririko wa dhima ya kukodisha | (8,529) | 26,720 |
| Gawio lililolipwa | (1,910,363) | (1,226,956) |
| **Fedha taslimu iliyotokana na mtaji** | **(4,076,733)** | **9,139,523** |
| **Cash and cash equivalents:** | | |
| **Jumla ya fedha taslimu za Mtiririko kwa mwaka** | **(4,463,719)** | **6,509,690** |
| Fedha na thamani ya fedha mwanzo wa mwaka | 6,704,875 | 195,185 |
| **Fedha na thamani ya fedha mwisho wa mwaka** | **2,241,156** | **6,704,875** |

## WASILISHO

Ndugu wanahisa mnaombwa kupokea na kuridhia taarifa ya Kampuni na taarifa ya fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 na kuazimia kama ifuatavyo.

# Azimio la 2/2025

*"Taarifa ya mwaka ya Wakurugenzi na taarifa ya fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia Desemba 2024 imepitishwa kama ilivyowasilishwa"*




WEKEZA
SASA NA
AFRIPRISE
INVESTMENT PLC.
11
132
319

Dondoo Na. 20/6/2025

## KUTANGAZA GAWIO

Kwa mwaka wa fedha ulioshia Desemba, 31 2024, Bodi inapendekeza kulipa gawio la shilingi 18 ikilinganishwa na gawio la  TZS 13 kwa mwaka 2023.

### WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa kama Mkutano Mkuu utaridhia pendekezo hili, malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike baada ya kupitisha azimio hili. Kwa wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatafanyika kupitia Akaunti zao, na kwa wale ambao hawana akaunti za benki malipo yatafanyika kwa njia ya mitandao ya simu.

# *Azimio la 3/2025*

*Mkutano Mkuu umeazimia, kuridhia pendekezo hili kwamba gawio la shilingi za Kitanzania Kumi na nane (18) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi.*



## UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2025

Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2024, mahesabu ya Kampuni yalikaguliwa na Kampuni ya Ukaguzi wa Mahesabu na Ushauri ya CROWE Tanzania.

CROWE Tanzania imehudumu kama mkaguzi wa nje wa Kampuni kwa kipindi cha miaka saba mfululizo. Kwa mujibu wa miongozo ya utawala bora na maadili ya taaluma ya uhasibu na ukaguzi, muda huu unatosha na Kampuni hiyo imefikia ukomo wa muda wa kukagua mahesabu ya Kampuni yetu. Hivyo, hawatateuliwa tena kuendelea na kazi hiyo kwa mwaka unaofuata.

Baada ya mchakato wa tathmini na mapendekezo kutoka Kamati ya Ukaguzi ya Bodi ya Wakurugenzi, Uditax International imechaguliwa kama kampuni mpya ya ukaguzi. Kampuni hii ina uzoefu wa kutosha, sifa stahiki na rekodi nzuri katika kutoa huduma za ukaguzi kwa makampuni yaliyosajiliwa katika soko la hisa.

### WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa **Auditax International**, wateuliwe kuwa Wakaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha unaoishia **Desemba 31, 2025.** Ada ya ukaguzi inayopendekezwa ni **Shilingi Milioni Ishirini na mbili (Shs 22,000,000/=)** kabla ya kodi.

Ada hii imezingatia mwenendo wa soko kwa taaluma ya uhasibu na ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni, uhitaji wa ukaguzi kwa kampuni iliyoorodheshwa katika soko la hisa, pamoja na mfumuko wa bei nchini.

Wanahisa **wanaombwa kuridhia pendekezo hili la Bodi katika Mkutano Mkuu wa Ishirini.**



## PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Malipo ya Wajumbe wa Bodi, [Directors fees] yameainishwa kwenye Katiba ya Kampuni. Kifungu Namba 70 [i] kinaeleza kuwa: “The remuneration of the Directors shall from time to time be determined by the Company in General Meeting”.Malipo haya huwa yanawekwa kwenye Bajeti ya Kampuni kila mwaka. Malipo ya Wajumbe yanatokana na ukweli kuwa Wajumbe wa Bodi hutumia muda mwingi kusimamia shughuli za Kampuni, badala ya kusimamia shughuli zao binafsi.

Ikumbukwe kuwa Wajumbe wa Bodi ndio wanawajibika kwa Mkutano Mkuu kwa kusimamia shughuli za Kampuni kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, pamoja na kanuni na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam, utawala bora na ufanisi wa Kampuni. Kwa kifupi chini ya Sheria ya Makampuni, Wajumbe wanawajibika kuhakikisha kuwa wanasimamia vema Kampuni ili wanahisa wasipoteze fedha zao na kwamba mtaji wa Kampuni unakua.

### WASILISHO

Kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2024, Menejimenti inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni sita na laki mbili (Shilingi 6,200,000).

## Azimio la 5/2025

*“Imeazimiwa kwamba kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni sita na laki mbili (Shilingi 6,200,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi.”*



Dondoo Na. 20/9/2025

## KUHUSU: UTOAJI WA HISA ZA UPENDELEO ZISIZO NA HAKI YA KUPIGA KURA ZENYE UWEZO WA KUKOMBOLEWA (ISSUANCE OF NON-VOTING REDEEMABLE CUMULATIVE PREFERENCE SHARES)

**IKUMBUKWE KUWA:**

Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Uwekezaji ya Afriprise, katika kikao chake cha kawaida, ilipitisha pendekezo la kutoa Hisa za upendeleo zisizo na Haki ya Kupiga Kura zenye uwezo wa kukombolewa, kupitia mpango wa Private Placement, kwa lengo la kukusanya mtaji wa jumla ya TZS bilioni 20 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati ya Kampuni.

**IKIZINGATIWA PIA KUWA:**

- Endoxa Law amependekezwa kuwa Mshauri wa Kisheria (Legal Advisor) kwa ajili ya mchakato huu;
- Mwekezaji anayelengwa ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF);
- Mapato yatakayopatikana kutoka kwenye mpango huu yatatumika katika:
    - Kuanzisha bidhaa mpya za kifedha ikiwemo Unsponsored Depository Receipts kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE);
    - Kuwekeza katika sekta ya viwanda kwa ushirikiano na taasisi za fedha kwa dhamana ya Benki Kuu ya Tanzania;
    - Kutoa mikopo kwa taasisi za fedha ndogo zilizosajiliwa (licensed microfinance institutions) kwa lengo la kuongeza ujumuishi wa kifedha.

**HIVYO BASI, WANAHISA WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA AFRIPRISE, WAKIWA KWENYE MKUTANO MKUU WA MWAKA, WANAAZIMIA IFUATAVYO:**

1. Kuridhia mpango wa utoaji wa Hisa za upendeleo zisizo na Haki ya Kupiga Kura zenye uwezo wa kukombolewa, zenye jumla ya thamani ya hadi TZS 20,000,000,000.00 kupitia mpango wa Private Placement.

2. Kuipa mamlaka Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Uwekezaji ya Afriprise kutekeleza mchakato wa utoaji wa hisa hizo, ikiwa ni pamoja na:
    - Kuingia mikataba na taasisi husika,
    - Kuwasilisha maombi kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA),
    - Kuandaa nyaraka zote muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu.

Wanahisa **wanaombwa kuridhia pendekezo hili la Bodi katika Mkutano Mkuu wa Ishirini.**

# KUFUNGA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI



## KIAMBATANISHO 1 - MAHUDHURIO

| SNO | JINA LA MWANAHISA | AINA YA UWAKILISHI | |
|---|---|---|---|
| 1 | ALEXANDER TONGORI MACHANGO | | MWANAHISA |
| 2 | BARTHOLOMEW MAJOR KUNZUGALA | | MWANAHISA |
| 3 | BONIFACE DONALD MAKERE | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | MWAKILISHI |
| 4 | CHARLES MALABA MBUSHI | | MWANAHISA |
| 5 | CYPRIAN GEOFREY MWELLAH | | MWANAHISA |
| 6 | DOMINIC DANIEL KYARUZI | | MWANAHISA |
| 7 | DORICE ADRIAN MAGAYANE | | MWANAHISA |
| 8 | DR. DOROTHY MARTIN MASOZA | | MWANAHISA |
| 9 | DR.TUMAINI EDWARD MHADA | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | MWAKILISHI |
| 10 | DR.VICENT ISAAC MHADA | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | MWAKILISHI |
| 11 | EVANS EDDY MLAY | | MWANAHISA |
| 12 | HILDA KOKULAMUKA TEGAMAISHO | LISIUS LADISLAUS | MWAKILISHI |
| 13 | JAMES MAJUKANO GEGE | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | MWAKILISHI |
| 14 | KANYENYE KISULILA MATANGA | | MWANAHISA |
| 15 | MICHAEL DANIEL KAVUTA | | MWANAHISA |
| 16 | MOHAMED BURHAN | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | MWAKILISHI |
| 17 | MWIDINI BAKARI MNALI | | MWANAHISA |
| 18 | SHABANI RAMADHAN ZAMBO | ADAM SHABAN ZAMBO | MWAKILISHI |
| 19 | TCCIA MOROGORO | | MWANAHISA |
| 20 | WINFRIDA ELIAB CHIDUO | | MWANAHISA |
| 21 | ABBASI EXPORTS LIMITED | BENEDICT MUSHI | MWAKILISHI |
| 22 | AGAPE AMADEUS KAMAGENGE | | MWANAHISA |
| 23 | ALEX FELIX MAJOH | | MWANAHISA |
| 24 | ALOYCE SANULA SWILA | | MWANAHISA |
| 25 | AZIZI HASSANI HARUNA | | MWANAHISA |
| 26 | BHAVIT KAMALNAYAN BHATIA | | MWANAHISA |
| 27 | BRIGHTON MANYAMA AIDAN | | MWANAHISA |
| 28 | CHRISTOPHER MWITA GACHUMA | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | MWAKILISHI |
| 29 | CLAUDI COSMAS MFUNGO | | MWANAHISA |
| 30 | COSMAS ADAM MKONDE | | MWANAHISA |
| 31 | DAYAN REUBEN OLEKUNEY | | MWANAHISA |
| 32 | DEOGRATIAS ATHANAS MROSSO | | MWANAHISA |
| 33 | DOMINIC BEDA MASSAWE | | MWANAHISA |
| 34 | ELISHA JOSEPH | | MWANAHISA |
| 35 | EMMANUEL JOHN CHINGO | | MWANAHISA |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 36 | ERICK ELIEZER BALIGE | | MWANAHISA |
| 37 | GASPAR KABACHUBYA MUNYAGI | | MWANAHISA |
| 38 | GODFREY MEITAMEI MOLLEL | FADHILI GODFREY MOLLEL | MWAKILISHI |
| 39 | GREGORY JOHN MUSHI | | MWANAHISA |
| 40 | HABAKUKI HUSSEN MAKAO | | MWANAHISA |
| 41 | HENRY GEORGE MBOTTO | | MWANAHISA |
| 42 | HERMAN PATRICK GOODLUCK | | MWANAHISA |
| 43 | HERY EDSON MWIDUNDA | | MWANAHISA |
| 44 | IGROWTH MANAGED FUND | FRANCIS SAMKYI | MWAKILISHI |
| 45 | IPYANA PHILBERT MWANKEMWA | | MWANAHISA |
| 46 | IRENE BAHOYA KULOLA | | MWANAHISA |
| 47 | ISARIA KAWEDI MWENDE | | MWANAHISA |
| 48 | IVO JULIUS MATEE | | MWANAHISA |
| 49 | JAVAN MUGANDA PERE | | MWANAHISA |
| 50 | JOAN JAMES MNGODO | | MWANAHISA |
| 51 | JONATHAN SHAURI KARAZE | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | MWAKILISHI |
| 52 | JOSEPH MARTINI NDEDELA | | MWANAHISA |
| 53 | JOYCE MWITA GACHUMA | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | MWAKILISHI |
| 54 | KELVIN LUCAS MALLYA | | MWANAHISA |
| 55 | LAURA SYLVESTER MATTUNDA | | MWANAHISA |
| 56 | LILIAN KOKUSHERULA NYOMBI | | MWANAHISA |
| 57 | LYAMBA, JULIUS NG`WANANNOGU | | MWANAHISA |
| 58 | MAANYA MOHAMED SOLISI | | MWANAHISA |
| 59 | MARY L MTAVANGU | | MWANAHISA |
| 60 | MASAIDA MUSSA CHIWINGA | | MWANAHISA |
| 61 | MASIMBA CLEMENT KAKA | | MWANAHISA |
| 62 | MNANKA GEBANI WINANI | | MWANAHISA |
| 63 | MWANZA COMMUNITY INVESTMENT PLC | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | MWAKILISHI |
| 64 | NATHAN EDWARD MNYAWAMI | | MWANAHISA |
| 65 | OGARA GABRIEL SASSI | | MWANAHISA |
| 66 | OMARY RUFUNGURO KUPERELWA | | MWANAHISA |
| 67 | PASCHAL PHINEHAS SARUNGI | | MWANAHISA |
| 68 | PASTOR PETRI MFOY | TIB RASILIMALI LTD | MWAKILISHI |
| 69 | PETER WILLIAM KIFUNGUOMALI | | MWANAHISA |
| 70 | PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND | HERMAN GOODLUCK | MWAKILISHI |
| 71 | RAMADHANI ZAIDI RUPIAH | | MWANAHISA |
| 72 | SARA DONALD MREMA | | MWANAHISA |
| 73 | SIMON JOHN KESSY | | MWANAHISA |
| 74 | STELLA MARO HIRJI | | MWANAHISA |
| 75 | STEVEN EMANUEL GOSSI | | MWANAHISA |
| 76 | SYNPHOROSE EVARIST BAITWA | | MWANAHISA |
| 77 | THERESIA SAMSON MUSHI | | MWANAHISA |
| 78 | VINCENT BERNARD MSAKI | | MWANAHISA |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 79 | WAHAB HASHIMU SHOO | | MWANAHISA |
| 80 | WARIALANGA AMOS MBISE | | MWANAHISA |
| 81 | YAKOBO MARUKUSI MAHAY | | MWANAHISA |
| 82 | ZUM SERVICES LIMITED | | MWANAHISA |
| 83 | PROF: LUCIAN MSAMBICHAKA | | MWANAHISA |
| 84 | MAGDALENA N. MKOCHA | | MWANAHISA |
| 85 | JOSEPH M. KAHUNGWA | | MWANAHISA |


AFRIPRISE
INVESTMENT PLC.
SAVE YOUR
TOMORROW, TODAY
BY INVESTING IN AFRIPRISE
Government Securities | NSE & RSE
Marketable Securities on DSE
Corporate Bonds
Fixed deposits.

LAYOUT & DESIGN:
INFINITY BRANDS (T) LTD
Mob: +255 624 400 295 | 717 200 295
E-mail: mudithan@mail.com

**AFRIPRISE INVESTMENTS PLC**
PSSSF Millenium Tower II, 24th Floor
P. O. Box 72678, Dar es Salaam, Tanzania
**Mobile:** +255 753 701 802 | **Email:** info@afriprise.co.tz
www.afriprise.co.tz